UJUMUISHWAJI WA VIJANA KATIKA MCHAKATO WA BAJETI TANZANIA: SAUTI AU UTUPU?

MUHTASARI

Ushirikishwaji na ujumuishwaji wa vijana katika mambo ya kijamii na hususan katika mchakato wa bajeti ni muhimu ili kuhakikisha mahitaji yao yanajulikana na kutafutiwa majibu; na kwamba tunaendelea kulinda Imani yao kwa jamii, amani iliyopo na utengamano wetu. Taarifa hii fupi ya kisera inachambua ushirikishwaji wa vijana katika mchakato wa bajeti hapa Tanzania, ikilenga uelewa wao wa mchakato wa bajeti, ushirikishwaji, uwakilishwaji, ujumuishwaji na Imani tuliyo nayo kwa vijana. Mambo yaliyoibuliwa yanatumika kama msingi wa mapendekezo ya kisera.

MAMBO MAKUU YALIYOIBULIWA

- Kuna uelewa, nia, ushirikishwaji na ujumuishwaji mdogo wa vijana katika mchakato wa bajeti.
- Taratibu zilizopo sasa, kama mfuko wa vijana katika ngazi ya serikali za mitaa unaotoa mikopo kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, hazikidhi mahitaji halisi ya vijana, hasa kukuza ubunifu,mawazo ya biashara na jitihada za kijana mmoja mmoja.
- Kuna Imani ndogo kwa vijana, katika taratibu na taasisi za serikali zinazohusika katika mchakato wa kuiidhinisha na kufuatilia bajeti kwa niaba ya jamii, kama bunge na Ofisi ya Mthibiti na Mkaguzi wa Mahesabu.
- Vijana hawaridhiki na sheria, taratibu na miongozo inayotumika kuhuisha uwajibikaji katika mzunguko wa bajeti.
- Taratibu za mawasiliano, sio rafiki kwa vijana, hivyo hazisaidii sana kuongeza ushirikishwaji wao, katika mchakato wa bajeti.
- Uzoefu wa Kenya na Vietnam, unaashiria kwamba kampeni zinazoongozwa na vijana, makongamano ya vijana, na wakati serikali za mitaa zinapochukua jukumu la kutafuta mchango wa vijana, na vilevile shughuli za serikali za mitaa zinapolenga jamii na kushirikisha vijana kutafuta suluhu ya changamoto za ushiriki wao, vinasaidia sana kuhamasisha vijana kushiriki katika shughuli za jamii, ikiwemo mchakato wa bajeti.

MAPENDEKEZO YA KISERA

- Kuandaa programu za kampeni kwa vijana za kuwajumuisha katika maandalizi, utekelezaji, na hata ukamilishaji wa bajeti, ili kupata matokeo mazuri zaidi.
- Kuanzisha makongamano mbalimbali (vijijini na mijini) ili kufungua majadiliano, na kutafuta maoni ya vijana; na vilevile kuwapa nyenzo na rasilimali muhimu.
- Kukuza ufungamanishaji wa sera, mipango na bajeti; na mahitaji ya vijana, hasa katika sekta za kipaumbele.
- Kuanzisha majukwaa ya kidigiti, chini ya wizara husika, kwa lengo la kukusanya maoni na ubunifu wa vijana na kuyafanyia kazi.
- Kufanya mapitio ya mitaala ya shule ili kuweka mafunzo ya ujumuishwaji katika mipango na mchakato wa bajeti kuanzia elimu ya msingi. Hii italazimu maafisa elimu kuhamasishwa na kupata mafunzo maalumu ya namna bora ya kutoa elimu hiyo.
- Serikali za mitaa zibuni na kutekeleza utaratibu unaoweka mbele jamii, katika shughuli zao.
- Kufanya mapitio ya mfumo wa serikali wa uwajibikaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya bajeti, kwa lengo la kuongeza Imani ya jamii, katika mchakato wa bajeti.

1. USULI NA UTANGULIZI

Kwa mujibu wa takwimu rasmi za serikali (2012 census), vijana (umri 15 - 35) ni asilimia 34.7 ya watanzania wote, wanaokadiriwa kufikia watu milioni 60. Ujumuishwaji wa vijana katika mambo ya jamii ikiwemo maandalizi ya bajeti, utelezaji wake, na ufuatiliaji na tathmini, ni muhimu. Bajeti kuwa jumuishi ni muhimu sana kwa maendeleo na kudumisha imani iliyojengeka kwa muda mrefu; na pia kudumisha amani na utengamano. Ushiriki wa makundi yasikuwa na sauti katika jamii, wakiwemo vijana na wanawake, katika mipango na taratibu za bajeti, ni jambo linalojadiliwa katika nchi nyingi. Kwa kawaida inachukuliwa kwamba watu wengi wana uelewa wa kutosha kuhusu mchakato wa bajeti, hivyo wanategemewa kushiriki. Mtazamo huu siyo sahihi, kama ilivyojitokeza katika mahojiano na vijana, na majadiliano ya vikundi vya vijana Tanzania. Taarifa hii inawasilisha mambo makuu yaliyoibuliwa na utafiti wa "Tanzania's Fiscal Governance, Budget, Needs and Public Expenditure with the analysis on inequalities and Trust." Hususan inaelezea kwa kifupi matokeo ya uchambuzi wa kina wa ushirikishwaji wa vijana katika mchakato wa bajeti; na kujifunza kutokana na uzoefu na mifano mizuri sehemu nyingine.

34.7 %

Uwiano wa vijana na idadi ya watu Tanzania



2. VIJANA TANZANIA NA MCHAKATO WA BAJETI – MAMBO MAKUU

Kwanza, utafiti ulizingatia demografia ya vijana walioshiriki katika zoezo hili na kutoa taarifa. Utafiti ulionesha kwamba wavulana wana uelewa mkubwa zaidi na wanashiriki zaidi katika mchakato wa bajeti ukilinganisha na vijana wenzao wanawake. Pia, vijana wasiokuwa na elimu kubwa wana ari zaidi ya kushiriki katika mambo ya jamii, ikiwemo mchakato wa bajeti, ukilinganisha na wenzao wenye kiwango cha juu cha elimu. Aidha, kinyume na matarajio, vijana vijijini wanashiriki zaidi katika mchakato wa bajeti, kupitia mikutano ya vijiji, kuliko wenzao wanaoishi mijini. Hata hivyo, bila kujali jinsia, kiwango cha elimu na makazi yao, vijana wengi wana uelewana na ari ndogo ya kushiriki katika mchakato wa bajeti. Wachache wenye uelewa wa taratibu za bajeti, wanaona zoezi zima kama jambo la kinadharia zaidi ambalo haliendani na uhalisia wa mambo; na kwa hiyo wanakosa hamasa ya kushiriki. Wanaamini mchakato wa bajeti haufungamani na kanuni za utawala bora kama uwazi, ushirikishwaji na uwajibikaji.

I. USHIRIKISHWAJI, UJUMISHWAJI, NA UWAJIBIKAJI KATIKA MCHAKATO WA BAJETI:

Vijana walilalamikia kutokushirikishwa, hali ya kujisikia kutengwa au mambo yao kutokujumuishwa, na hatua hafifu za uwajibikaji zilizopo.

Ushirikishwaji	Ujumuishwaji	Uwajibikaji
• Kukosekana kwa majukwaa huru yasiyoegemea upande wowote ili kuwawezesha kutoa maoni yao. • Kuminywa kwa uhuru wa kujieleza hapa nchini. • Njia pendwa za mawasiliano kama mitandao ya jamii na tovuti kutopewa umuhimu.	• Malalamiko na mahitaji kutokufanyiwa kazi na mamlaka husika. • Vijijini, wazee kupewa uzito ukilinganisha na vijana kutokana na mila na desturi zetu. • Kutokuwepo kwa utaratibu wa wazi wa ushirikishwaji wa vijana. • Maelekezo kwa serikali za mitaa ya kutenga 10% ya bajeti kwa wanawake na vijana hayaheshimiki.	• Uwajibikaji tata na usioaminika hasa kwa ngazi za chini. • Vyama vya siasa kuingilia kati suala la uwajibikaji katika utekelezaji wa bajeti. • Uwajibikaji binafsi wa maafisa wanaosimamia utekezaji wa bajeti unatia shaka. • Adhabu kwa maafisa wanaoshindwa kuwajibika ni ndogo mno.

II. UWAZI, IMANI NA UPATIKANAJI:

Kwa mujibu wa vijana, mchakato wa bajeti kwa ujumla hauaminiki. Vijana wanauona kama wa kinadharia zaidi kwa sababu utekelezaji wake unaonekana kutokuenda sambamba ya bajeti yenyewe. Kukosekana kwa uwazi katika mchakato wa bajeti ndiyo kikwazo kikuu katika jitihada za kujenga imani kwenye mchakato mzima.

Uwazi	Imani	Upatikanaji
• Makundi yasiyokuwa na sauti katika ngazi ya chini kabisa hayafaidiki kama bajeti zinavyoonesha, na wala hakuna anaeelezea tofauti hii. • Maelezo ya tofauti kati ya bajeti inayoidhinishwa na fedha zinazotolewa hayatolewi. • Utaratibu wa kupata ripoti za serikali zilizokaguliwa siyo wazi kwa jamii.	• Kijana mmoja alisema "bajeti inaongezeka kila mwaka lakini thamani ya nyongeza ya matumizi haionekani (value for money). • Wawakilishi wa sasa katika mchakato wa bajeti kama vile Wabunge, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, na Mhasibu Mkuu wa Serikali, hawaaminiki na jamii.	• Lugha na mtindo unaotumika kwa maandalizi ya bajeti na ripoti za ufuatiliaji na tathmini havieleweki kwa watu wa kawaida mitaani. • Upatikanaji wa fedha zinazotengwa kwa vijana kupitia LGAs na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi (NEEC), ni changamoto. • Ripoti za ukaguzi hazipatikani kwa kwa watu wanaopenda kufuatilia hoja za ukaguzi

Hata hivyo, kutojali na ushirikishwaji mdogo katika shughuli za jamii hususan katika taratibu za bajeti, ni jambo linaloikumba jamii yote. Tayari mfumo wa elimu una masomo kama vile stadi za kazi, elimu ya uraia, elimu ya jumla na elimu ya maendeleo. Masomo haya yakifundishwa vizuri yanaweza kuongeza uelewa wa vijana, na ushiriki wao katika mambo ya jamii na katika mchakato wa bajeti. Changamoto in kwamba, hata wanaosimamia shule, na waalimu, ni sehemu ya jimii; kwa hiyo wanaweza kukosa ari au hamasa ya kushirikisha wanafunzi, kwenye mambo ya jamii. Jambo hili linahitaji semina maalumu za waalimu ili kukuza uelewa wao wa umuhimu wa jambo hili, na pia wajibu wao wa msingi wa kuelimisha vijana na jamii kwa ujumla.

3. MIFANO MIZURI YA KUIGWA KUHUSU UJUMUISHWAJI WA VIJANA – MAFUNZO KUTOKA KENYA NA VIETNAM

I. KENYA (NCHI JIRANI)



Mwaka 2019, Davanne wa Benki ya Dunia, aliandika makala kuhusu Kenya wanavyowawezesha vijana kushiriki katika mchakato wa bajeti. Kwa mujibu wa Makala hayo, mambo mengi yanayodumaza ushiriki wa vijana katika mchakato wa bajeti Kenya, yanawiana ya mambo yaliyoibuliwa katika taarifa hii. Matokeo mazuri zaidi yalipatikana wakati Kenya ilipoanzisha utaratibu wa kugatua madaraka kwa serikali za majimbo na kuyafanya kuwa na majukumu zaidi ya kusimamia mahitaji ya jamii zao. Kenya ilianza kutekelekeleza mpango wa -Open Government Partnership, wakifanya kazi kwa karibu na mradi wa -World Bank's Kenya Accountable Devolution Program (KADP).

© OpenStreetMap's contributors

II. VIETNAM (MFANO WA KUIGWA WA MAGEUZI YA UCHUMI)

Vietnam, ambayo ilikuwa na changamoto zinazofanana na za Kenya na Tanzania, ilianzisha kampeni zilizoongozwa na vijana kuchochea mipango shirikishi na uwazi katika bajeti (Oxfam, 2019). Utaratibu wao ulijikita katika kujenga uwezo na kuandaa kampeni za uelewa kupitia mitandao. Ili kufanikisha programu yao walijifunza jinsi vijana wanavyofikiri na kupokea mambo; na hivyo walianza mikakati kama vile kufikia mwafaka; hoja, mapendekezo na kampeni zinazoongozwa na vijana; na kufanya tathmini ya mara kwa mara. Mradi huu ulisaidia kubuni programu mathubuti za vijana, namna ya kufanya kazi nao, na kuwapa fursa za kuongoza, ili kuongeza ushiriki wao katika maendeleo ya jamii.



© OpenStreetMap's contributors

III. MAFUNZO KUTOKANA NA UZOEFU WAO:

- Serikali za mitaa zibuni na kutekeleza utaratibu unalenga jamii na kujumuisha vijana katika mchakato wa bajeti.
- Kuwepo na makongamano (vijijini na mijini) ya mijadala ya kupata maoni ya vijana na kuwapa nyenzo na rasilimali muhimu.
- Kufanya kazi moja kwa moja na vijana ya kubuni taratibu mahiri, na kupata suluhu ya ushiriki wao, na vilevile kuwapa hamasa ya kushiriki katika mchakato wa bajeti.
- Ofisi husika za serikali ziandae mikutano, na kuomba michango ya vijana katika majukwaa yanayowafikia, kwa kuzingatia hali ya vijijini na mijini.
- Kuandaa programu za kampeni za vijana na kuwashirikisha katika maandalizi, utekezaji, na hata kuzihitimisha ili kupata matokeo mazuri zaidi.

4. MWISHO

Vijana ni sehemu kubwa ya idadi ya watu katika nchi nyingi zinazoendela ikiwemo Tanzania. Mchakato shirikishi wa bajeti ni muhimu ili kukuza ushiriki wa vijana katika shughli za jamii. Vijana wanaposhawishika na kutamani kushiriki katika shughuli za maendeleo ya jamii, na wakajisikia kwamba mchango wao unathaminiwa, wanaongeza hamasa ya kuwekeza katika maendeleo ya nchi yao.

5. MAPENDEKEZO YA VIJANA

- Kuwepo na programu za kuelimisha na kujenga uwezo wa vijana hususan katika mipango na taratibu za bajeti.
- Watu muhimu na wenye maamuzi katika mchakato wa bajeti, wapewe mafunzo kuhusu umuhimu wa kujumuisha vijana, ili wabuni mikakati mizuri ya kuwashirikisha.
- Kuna haja ya kuwa na vikundi vya majadiliano vya vijana katika ngazi tofauti, na kwa mambo mtambuka.
- Kuendelea kuwianisha sera, mahitaji na matarajio ya vijana.
- Kujumuisha vijana kupitia njia rafiki za mawasiliano kama vile mitandao ya kijamii, tovuti nk.,
- Ujumuishwaji wa vijana katika shughuli za jamii, ikiwemo bajeti, iwe ni mojawapo ya mafunzo muhimu katika mfumo wa elimu, kuanzia elimu ya msingi.
- Utaratibu wa bajeti upewe uzito kama ilivyo kwa mchakato wa uchaguzi.
- Adhabu kwa kushindwa kusimamia vizuri utekelezaji wa bajeti, au matumizi mabaya ya fedha za umma, iwe kubwa, ili iwe fundisho.
- Sheria zinazosimamia taratibu za uwajibikaji na adhabu, ziangaliwe upya.

MTAFITI MKUU

Prof. Marcellina Mvula Chijoriga ni profesa mstaafu wa mambo ya fedha na menejimenti ya biashara. Alihudumu katika Taasisi ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (University of Dar es Salaam Business School -UDBS) kwa miaka 36. Ni mkufunzi mbobezi, mtafiti na mshauri mtaalamu wa biashara za umma na binafsi. Pia alikuwa mjumbe wa bodi mbalimbali na Taasisi kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania na Shirika la Fedha Duniani -IMF. Kwa sasa ni Afisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya LOGIMAC Ltd.